JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

PROGRAMU YA JENGA KESHO ILIYO BORA (BUILDING A BETTER TOMORROW - BBT) 2022 - 2030

MWONGOZO NA.1: UTOAJI MAFUNZO KATIKA VITUO ATAMIZI NA UENDESHAJI WA MASHAMBA MAKUBWA YA PAMOJA YA BBT (BBT BLOCK FARMS)

MACHI 2023

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

MWONGOZO NA.1: UTOAJI MAFUNZO KATIKA VITUO ATAMIZI NA UENDESHAJI WA MASHAMBA MAKUBWA YA PAMOJA YA BBT (BBT BLOCK FARMS)

Umeandaliwa na:
Wizara ya Kilimo,
S.L.P 2182,
DODOMA.

DIBAJI

Sekta ya kilimo ni mhimili wa uchumi wa nchi yetu na inachangia pato la mkulima mmoja mmoja, Kaya na Taifa kwa ujumla. Sekta hii kwa mwaka 2022 imechangia asilimia 26.1 ya Pato la Taifa, imetoa ajira za moja kwa moja kwa wananchi kwa wastani wa asilimia 65.6, imechangia asilimia 65 za upatikanaji wa malighafi za viwanda na imechangia usalama wa chakula kwa zaidi ya 100%.

Kutokana na changamoto ya ukosefu wa ajira, mitaji na mtazamo hasi wa vijana kwenye kilimo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeanzisha programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (Building a Better Tomorrow – BBT) inayolenga kupunguza changamoto ya ajira na kuhamasisha ushiriki wa vijana katika kilimo kwa kuwapatia mafunzo, maeneo ya mashamba, mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko.

Ili kuhakikisha malengo ya uanzishaji wa Programu hii yanafanikiwa, Wizara imeandaa Mwongozo wa Mafunzo, Uendeshaji na Usimamizi wa mashamba makubwa ya pamoja. Mwongozo huu unatoa dira ya namna programu inavyoendeshwa na wajibu wa kila kundi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa program.

Wakati wa uzinduzi wa Programu ya BBT na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania mwezi Machi 2023 programu ilikua na mashamba ekari 300 na mpaka sasa mashamba ya program ni zaidi ya ekari 200,000.

Fedha zinazowekezwa kwenye program hii ni fedha za umma. Ni matarajio ya Wizara kuwa yeyote atakayepata fursa ya kushiriki na kunufaika na uwekezaji huu, anawajibu wa kuhakikisha anaitunza miundombinu iliyowekezwa.

Ni matumaini yangu kwamba Mwongozo huu utaongeza uwajibikaji, ufanisi na uelewa katika kuratibu utekelezaji wa programu na kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo na kukuza ajira.

HUSSEIN M. BASHE (Mb)

WAZIRI WA KILIMO

SHUKRANI

Serikali inaendelea kufanya juhudi za makusudi kuongeza ushiriki wa vijana na wanawake katika sekta ya kilimo kwa kuwa asilimia 34 ya Watanzania ni vijana ambao ndiyo nguvu kazi kubwa ya Taifa.

Katika mwaka 2023 Serikali imesajili wa vijana wenye nia ya kushiriki katika shughuli za kilimo na kuwapatia mafunzo ya kilimo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu katika mnyororo wa thamani wa mazao katika vituo atamizi vilivyopo chini ya Wizara ya Kilimo.

Ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa Program hii, Wizara imeandaa mwongozo utakaotoa dira ya Utoaji wa mafunzo, Usimamizi, Uwekezaji na Uendeshaji wa mashamba makubwa ya pamoja (block farming) chini ya Progaramu ya BBT.

Ninawashukuru wadau wote walioshiriki katika zoezi la kuandaa mwongozo huu ambao unatoa maelekezo ya namna ya kusimamia utekelezaji wa programu ya BBT na kuongeza uzalishaji na tija katika maeneo ya mashamba ya BBT ili kukuza uchumi na kuongeza pato kwa vijana na Taifa kwa ujumla. Shukrani za dhati kwa Ofisi ya Uratibu ya Program ya BBT, Idara ya Sera na Mipango, Mafunzo na Utafiti, Maendeleo ya Mazao, Usimamizi na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya

Kilimo, Utawala na Rasilmali watu, Kitengo cha Sheria, na Wadau wa Maendeleo katika kujitoa kuhakikisha mwongozo huu unakamilika kwa wakati.

Gerald G. Mweli, *ndc*

KATIBU MKUU

YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI.....1
2.0 LENGO LA MWONGOZO 3
2.1 Lengo Kuu 3
2.2 Malengo Mahsusi ya Mwongozo 3
2.3 Umuhimu wa Mwongozo 3
3.0 MWONGOZO WA UENDESHAJI WA MASHAMBA MAKUBWA YA PAMOJA YA BBT (BBT BLOCK FARMS) 4
3.1 UDAHILI WA VIJANA KWAAJILI YA KUJIUNGA NA PROGRAMU YA BBT 4
3.1.1 Sifa za Kujiunga 4
3.1.2 Taratibu za Kujiunga 5
3.1.3 Taratibu na Kanuni za Mafunzo katika Vituo Atamizi 5
3.1.4 Vigezo na Masharti kwa Washiriki katika Vituo Atamizi vya Kilimo Biashara 6
3.1.5 Kanuni na Taratibu za Kufuata katika Vituo Atamizi vya Mafunzo ya Kilimo Biashara 6
3.2 UPATIKANAJI NA UGAWAJI WA MASHAMBA 6
3.2.1 Upatikanaji wa Mashamba 7
3.2.2 Ugawaji wa Mashamba 7

3.2.2.1 Mashamba kwa wanufaika wa Programu ya BBT 7

3.2.2.2 Ugawaji wa mashamba ya BBT kwa Wawekezaji 9

3.2.2.3 Utaratibu wa Kumpata Mwekezaji 10

3.3 UENDESHAJI WA MASHAMBA YA BBT 10

3.4 MAJUKUMU YA WADAU 11

3.4.1 Majukumu ya Wizara ya Kilimo 11

3.4.2 Majukumu ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 12

3.4.3 Majukumu ya Sekta Binafsi na Wabia wa Maendeleo 13

3.4.4 Majukumu ya Mwekezaji katika mashamba ya BBT 13

3.4.5 Majukumu ya Chama cha Ushirika 15

3.4.6 Majukumu ya Wanufaika wa Program ya BBT (Vijana) 15

3.5 SABABU ZINAZOWEZA KUMWONDOA KIJANA KWENYE PROGRAMU YA BBT 17

4.0 HITIMISHO 18

KIAMBATISHO NA. 1 19

KIAMBATISHO NA. 2 20

KIAMBATISHO NA. 3 21

1.0 UTANGULIZI

Sekta ya Kilimo ni mhimili wa uchumi wa Tanzania ambapo katika mwaka 2021/2022 imechangia asilimia 26.1 ya pato la Taifa, asilimia 65 ya malighafi za viwanda na asilimia 65.6 ya ajira. Aidha, mazao ya kilimo yamechangia takriban Dola za Marekani Bilioni 1.38 katika mwaka 2021/2022 kutokana na mauzo nje ya nchi (Tathmini ya Hali ya Uchumi 2021/2022).

Kutokana na matokeo ya Sensa ya kilimo ya mwaka 2020, takwimu zinaonesha kuwa Tanzania bara ina jumla ya Kaya 11,659,589. Kati ya hizo, Kaya 5,088,135 zinategemea kilimo moja kwa moja ambazo ni sawa na asilimia 43.6 ya Kaya zote. Aidha, idadi ya watu inatarajiwa kuongezeka kutoka milioni 61.74 mwaka 2022 hadi kufikia watu Milioni 80 mwaka 2030 na mwaka 2050 watu Milioni 136. Makadirio ya mahitaji ya chakula ifikapo mwaka 2030 yatakuwa tani milioni 20 na ifikapo mwaka 2050 yatafikia tani milioni 33.7. Katika kuhakikisha usalama wa chakula na lishe pamoja na kuimarisha biashara ya mazao ya kilimo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa kilimo imepanga kuweka mikakati ya uwekezaji wa muda mrefu kwenye Sekta ya Kilimo.

Tanzania inakadiriwa kuwa na vijana milioni 16 walio na umri wa miaka kati ya 10 hadi 15 na vijana milioni 6 wenye umri kati ya miaka 25 hadi 34. Hii ina maana kuwa, nchi ina hazina kubwa ya nguvu kazi kwa ajili ya kuzalisha chakula cha kutosha na ziada kuuzwa nje ya nchi. Hata hivyo, ushiriki wa

vijana katika Sekta ya Kilimo ni mdogo kutokana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na: mtazamo hasi kwa vijana na wanawake kuhusu kilimo na fursa za kibiashara zilizopo; ukosefu wa mitaji, ardhi, elimu na ujuzi katika kilimo biashara; kukosekana mfumo maalum wa kuwaunganisha na kuwahamasisha vijana kushiriki katika kilimo biashara; vijana kukosa vigezo vinavyowezesha kupata mikopo kutoka taasisi za kifedha; na kukosekana kwa masoko ya uhakika kwa mazao ya kilimo.

Katika kutatua changamoto hizo na kuwawezesha vijana na wanawake kushiriki katika kilimo, Wizara ya Kilimo imeanzisha programu ya kuwezesha ushiriki wa vijana na wanawake katika Kilimo Biashara (Building a Better Tomorrow - BBT). Malengo ya utekelezaji wa program hii ni: Kuwezesha na kuongeza Ushiriki wa Vijana na Wanawake katika Kilimo Biashara ili kuwapatia ajira; Kuongeza tija; Kuimarisha usalama wa chakula; Kuongeza mchango wa Sekta ya kilimo kwenye Pato la Taifa (GDP); na Kuinua hali ya maisha ya jamii ya Watanzania.

Utekelezaji wa program ya BBT unahusisha Mashamba Makubwa ya Pamoja (Block Farms); Huduma za Ugani; Uchimbaji wa Visima vya Umwagiliaji na Mikopo yenye riba nafuu kwa vijana na wanawake. Kwa upande wa mashamba makubwa ya pamoja utekelezaji umeanza kwa kugawa mashamba kwa vijana na wanawake kwa kuzingatia aina ya mazao yatakayozalishwa, upatikanaji wa mashamba, hali ya

afya ya udongo, ikolojia ya eneo husika na upatikanaji wa masoko. Ili kufikia malengo ya Programu hii ikiwemo kuongeza tija, kunahitaji usimamizi madhubuti na uwajibikaji kwa wadau wote. Ni muhimu kuwepo na usimamizi mathubuti kwa ajili ya uendelezi wa programu. Hivyo, Serikali imeandaa mwongozo wa uendeshaji wa programu ya BBT.

2.0 LENGO LA MWONGOZO

2.1 Lengo Kuu

Mwongozo huu umeandaliwa ili kutoa dira ya Utoaji wa mafunzo, Usimamizi, Uwekezaji na Uendeshaji wa Mashamba Makubwa ya Pamoja (block farming) chini ya Programu ya BBT.

2.2 Malengo Mahsusi ya Mwongozo

i. Kuainisha taratibu za upatikanaji wa vijana wanaojiunga na program;
ii. Kuweka taratibu za upatikanaji na Upangishaji wa Mashamba kwa wanufaika;
iii. Kuweka utaratibu wa uzalishaji wa mazao katika Mashamba Makubwa ya Pamoja; na
iv. Kuainisha haki, wajibu na majukumu ya wadau katika Programu BBT.

2.3 Umuhimu wa Mwongozo

Mwongozo huu ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha uendelevu wa program ya BBT ikiwemo upatikanaji wa

rasilmali, wajibu wa wadau mbalimbali na namna bora ya kusimamia utekelezaji wa program.

3.0 MWONGOZO WA UENDESHAJI WA MASHAMBA MAKUBWA YA PAMOJA YA BBT (BBT BLOCK FARMS)

3.1 UDAHILI WA VIJANA KWAAJILI YA KUJIUNGA NA PROGRAMU YA BBT

3.1.1 Sifa za Kujiunga

Vijana na wanawake watakaojiunga na Programu ya BBT wanapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka kati ya 18 hadi 40;

ii. Awe tayari kujifunza na kushiriki katika shughuli za kilimo biashara;

iii. Awe mwenye elimu angalau ya shule ya msingi;

iv. Awe tayari kuwa mfano kwa vijana wengine;

v. Awe hajaajiriwa katika mfumo rasmi wa ajira;

vi. Awe anayependa kushirikiana na wenzake;

vii. Awe na akili timamu;

viii. Awe mwenye tabia njema, mtiifu, mwenye nidhamu, mchapa kazi, mwaminifu na anayependa kuona matokeo chanya; na

ix. Awe tayari kuingia mkataba wa makubaliano baina yake na Serikali.

3.1.2 Taratibu za Kujiunga

Wizara ya Kilimo itatoa utaratibu kwa ajili ya waombaji wenye nia ya kijiunga na Programu ya BBT kuomba nafasi hizo. Waombaji wenye sifa za kijunga na BBT watapaswa kuwasilisha maombi yao kupitia utaratibu utakaowekwa kwa wakati husika ambapo uchambuzi utafanywa na timu ya wataalam wenye weledi itakayoteuliwa kwa ajili ya zoezi hilo. Vijana na wanawake wenye vigezo watapata mafunzo ya kilimo biashara na Uzalendo kwa utaratibu utakaobainishwa ikiwemo kupata mafunzo kupitia Vituo Atamizi (Incubation Centres) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Mafunzo hayo yatafanyika kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu (3).

3.1.3 Taratibu na Kanuni za Mafunzo katika Vituo Atamizi

Uendeshaji wa mafunzo ya kilimo biashara kupitia vituo atamizi utashirikisha Vijana Washiriki, Wakufunzi, Taasisi za Kifedha, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara za Kisekta na Taasisi zake, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia. Mfumo huu shirikishi utazingatia yafuatayo:

i. Uandaaji na usimamizi wa uendeshaji wa mafunzo ya kilimo biashara;

ii. Kuweka mazingira wezeshi ya uendeshaji wa mafunzo kwa vijana ikiwa ni pamoja na majengo (madarasa, mabweni,

ofisi, bwalo la chakula), miundombinu ya shambani, vitalu nyumba, uwekaji wa mifumo ya umwagiliaji na miundombinu ya kuhifadhi mazao baada ya kuvuna;

iii. Uwepo wa rasilimali fedha za kuwezesha kuanzisha na kuendesha mafunzo ya kilimo biashara kwa vijana; na

iv. Uwepo wa usafiri kwa ajili ya vijana kuweza kufanya ziara za mafunzo maeneo mbalimbali.

3.1.4 Vigezo na Masharti kwa Washiriki katika Vituo Atamizi vya Kilimo Biashara

Kijana atakaye kuwa amechaguliwa kujiunga na mafunzo katika vituo Atamizi atatakiwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyoainishwa kwenye **Kiambatisho Namba 1**.

3.1.5 Kanuni na Taratibu za Kufuata katika Vituo Atamizi vya Mafunzo ya Kilimo Biashara

Kijana atakaye kuwa amechaguliwa kujiunga na mafunzo atatakiwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizoainishwa kwenye **Kiambatisho Namba 2.**

3.2 UPATIKANAJI NA UGAWAJI WA MASHAMBA

Upatikanaji na ugawaji wa mashamba katika Programu ya BBT utazingatia aina ya mazao yatakayozalishwa pamoja na upatikanaji wa mashamba katika maeneo mbalimbali.

3.2.1 Upatikanaji wa Mashamba

Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR TAMISEMI) kupitia Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa itafanya utambuzi wa maeneo yanayofaa kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo. Maeneo hayo yatapimwa ukubwa, hali ya afya ya udongo pamoja na tathmini ya upatikanaji wa maji ili kuanisha aina ya mazao yatakayozalishwa.

Mazao yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na mazao yanayokomaa kwa muda mfupi kuanzia miezi mitatu hadi sita na mazao yenye thamani kubwa (*high value crops*). Mazao hayo ni ya bustani (horticulture) yanayojumisha mazao ya mbogamboga, matunda na viungo; mazao jamii ya mikunde (soya); mazao ya nafaka na mbegu za mafuta (alizeti).

Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, OR TAMISEMI, Sekta binafsi na Wabia wa maendeleo itaweka miundombinu muhimu kwenye mashamba hayo kwa ajili ya uzalishaji.

Vigezo vitakavyotumika kuchagua mazao ya kipaumbele katika eneo husika ni pamoja na: Hali ya afya ya udongo; Ikolojia ya eneo husika; na Upatikanaji wa soko.

3.2.2 Ugawaji wa Mashamba

3.2.2.1 Wanufaika wa Programu ya BBT

Ugawaji na ukubwa wa shamba kwa vijana na wanawake chini ya Programu ya BBT utazingatia mambo yafuatayo:

i. Awe amehitimu mafunzo muhimu ya BBT kulingana na utaratibu na vigezo vilivyowekwa;

ii. Aina ya zao litakalo zalishwa katika eneo husika;

iii. Aina ya mfumo wa uzalishaji utakaotumika (vitalu nyumba, mashamba ya wazi);

iv. Aina ya teknolojia ya uzalishaji;

v. Mpango kazi wa biashara wa kuendeleza zao husika kwa mnufaika;

vi. Awe hana ardhi ya uzalishaji;

vii. Aina na muda wa utumiaji wa ardhi (sub leasing); na

viii. Utayari wa kushiriki uzalishaji wa mazao katika mashamba ya BBT kwa kuzingatia kanuni bora na taratibu za upangishwaji wa ardhi kulingana na masharti yatakayotolewa kwa wakati husika.

Kwa vijana watakaozalisha mazao ya bustani watapewa mashamba yenye ukubwa wa kuanzia ekari 1 hadi 5 kutokana na mazao hayo kuzalishwa zaidi ya mara mbili kwa mwaka na kutegemea teknolojia inayotumika. Hivyo, vijana watakaozalisha kwa mfumo wa vitalu nyumba watapewa eneo sawa au dogo ikilinganishwa na uzalishaji wa kawaida. Aidha, kwa mazao jamii ya mafuta na mazao ya nafaka vijana watapewa eneo lenye ukubwa wa ekari lisilozidi ekari 10 kutokana na mazao hayo kuhitaji eneo kubwa zaidi ili kupata faida ikilinganishwa na mazao ya bustani.

Ili kuwa na uwajibikaji katika shughuli za uzalishaji na kuwezesha Wizara kuwa na usimamizi, vijana wanapaswa kufanya shughuliza kilimo chini ya Chama cha Ushirika kitakaouundwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za sheria ya ushirika nchini.

3.2.2.2 Ugawaji wa mashamba ya BBT kwa Wawekezaji

Ili kuimarisha uwekezaji, uongezaji thamani, ajira na masoko kupitia mashamba makubwa ya BBT, Serikali itatoa fursa kwa wawekezaji wakubwa wa kimkakati kuomba mashamba ya uwekezaji chini ya programu ya BBT. Sifa za Mwekezaji katika mashamba ya BBT ni pamoja na:

i. Uzoefu katika uzalishaji wa mazao, uongezaji thamani, ununuzi mazao na utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima;

ii. Uthibitisho wa Uwezo (Mitambo ya uandaaji, uzalishaji, uchakataji nk) wa kuendeleza ardhi ya kilimo kuanzia ekari 1,000;

iii. Uthibitisho wa mtaji wa uwekezaji (proof of own investment or financial guarantees);

iv. Awe na Mpango wa Biashara;

v. Awe tayari kuzalisha mazao yaliyoelekezwa na Wizara;

vi. Utayari wa kulipa kodi, ushuru na tozo mbalimbali za Serikali ikiwemo kodi ya ardhi (land rent), ushuru wa mazao na kodi nyingine za Serikali kwa mujibu wa sheria;
vii. Awe tayari kununua mazao yatakayozalishwa na vijana katika shamba alilowekeza; na
viii. Awe tayari kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi katika uwekezaji wake.

3.2.2.3 Utaratibu wa Kumpata Mwekezaji

Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika na uwekezaji itatangaza fursa kwa wawekezaji kwenye mashamba ya BBT.

3.3 UENDESHAJI WA MASHAMBA YA BBT

i. Mashamba ya BBT (BBT Block Farms) yatakuwa chini ya chama cha ushirika utakaoundwa na wanufaika wa Programu ya BBT katika shamba husika.
ii. Kila shamba litakuwa chini ya chama kimoja cha ushirika.
iii. Uanzishwaji wa chama cha Ushirika utazingatia Sheria ya Chama cha Ushirika (CAP.337 R.E 2002) na marekebisho yake ya Sheria Mbalimbali (Na.3) ya 2019;
iv. Usimamizi na Udhibiti wa Chama cha Ushirika kilichoundwa yatajumuishwa katika Sheria Ndogo, Kanuni, na miongozo mingine itakayotengenezwa na wanachama wa chama husika; na
v. Vijana kuanzisha miradi kupitia ushirika.

3.4 MAJUKUMU YA WADAU

3.4.1 Majukumu ya Wizara ya Kilimo

Katika kuendeleza programu ya BBT Wizara ya Kilimo itafanya yafuatayo:

i. Kudahili vijana wenye sifa kujiunga na Program ya BBT;

ii. Kutoa mafunzo ya kilimo biashara kwa vijana kabla ya kuanza uzalishaji kwenye mashamba makubwa;

iii. Kuratibu upatikanaji wa mashamba na kuweka taratibu za upangishwaji;

iv. Kuandaa mashamba ikihusisha kusafisha, Kupima afya ya udongo na kuweka miundombinu ya umwagiliaji na miundombinu mingine muhimu;

v. Kuwaunganisha vijana na masoko kupitia chama chao cha ushirika;

vi. Kuratibu upatikanaji wa wawekezaji katika mashamba ya BBT kwa kushirikiana mamlaka husika;

vii. Kuwapatia makazi kwa kipindi cha upangishaji wa shamba;

viii. Kuwapatia huduma muhimu ikiwemo chakula na huduma ya afya kabla ya kupata mavuno ya kwanza;

ix. Kushirikisha Wizara za Kisekta katika utekelezaji wa Programu ya BBT ili kuwezesha upatikanaji wa huduma

muhimu ikiwemo ardhi, maji, umeme, Barabara, huduma ya afya na elimu;

x. Kuwatambulisha vijana kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ya maeneo yalipo mashamba;

xi. Kushirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) katika kutoa mafunzo ya ukakamavu na uzalendo kwa vijana wa BBT;

xii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Programu ya BBT;

xiii. Kuhakiki na kutoa taarifa zinazohusu Programu ya BBT; na

xiv. Kuwaunganisha vijana na taasisi za fedha.

3.4.2 Majukumu ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinawajibu wa kutekeleza yafuatayo:

i. Kubainisha maeneo kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya BBT na kuwezesha upatikanaji wa hati;

ii. Kufuatilia maendeleo ya shughuli za kilimo zinazofanywa na vijana katika Programu ya BBT kwenye mikoa yao; na

iii. Kuhakikisha amani, usalama na utulivu kwenye mashamba ya BBT.

3.4.3 Majukumu ya Sekta Binafsi na Wabia wa Maendeleo

Wajibu wa Sekta Binafsi na Wabia wa Maendeleo ni pamoja na:

i. Kushirikiana na Wizara katika kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Programu;

ii. Kushiriki katika kuwezesha upatikanaji wa teknolojia, pembejeo za kilimo na masoko;

iii. Kushiriki katika kuweka miundombinu ya kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa;

iv. Kusaidia kutoa mafunzo ya namna ya kutunza hesabu na fedha.

v. Kushirikisha Wizara kwenye utekelezaji wa miradi yote inayohusisha Programu ya BBT; na

vi. Kutoa taarifa ya utekelezaji wa miradi yote inayohusisha program ya BBT kila mwisho wa mwaka wa Serikali.

3.4.4 Majukumu ya Mwekezaji katika mashamba ya BBT

Wajibu wa Wawekezaji katika mashamba makubwa ni pamoja na:

i. Kuendeleza eneo la shamba alilopangishwa kwa kuzingatia masharti ya mkataba;

ii. Kununua mazao yaliyozalishwa na vijana katika shamba (offtaking) kwa mujibu wa makubaliano;

iii. Kuwezesha upatikanaji wa huduma za ugani na huduma nyingine kama mitambo ya kusafisha na kuandaa mashamba na pembejeo za kilimo kwa vijana wa BBT katika shamba alilowekeza;

iv. Kurejesha shamba endapo atashindwa kuendelea na uzalishaji kwa kuzingatia masharti ya mkataba;

v. Kutekeleza na Kuzingatia taratibu na maelekezo yote yatakayotolewa na Serikali katika uendelezaji wa mashamba hayo;

vi. Kulipa kodi, ushuru na tozo mbalimbali za Serikali ikiwemo kodi ya ardhi (land rent), ushuru wa mazao na kodi nyingine za Serikali kwa mujibu wa sheria;

vii. Kutopangisha shamba kwa mtu binafsi, taasisi au Kampuni katika kipindi chote cha mkataba wa upangishaji;

viii. Kutunza na kuhifadhi mazingira katika eneo la utekelezaji wa Programu ikiwemo udhibiti wa taka (viuatilifu na vifungashio vyake, vifungashio vya mbolea, mabaki ya mazao, vyakula), matumizi bora ya maji, nishati nk; na

ix. Kutekeleza na Kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Serikali.

3.4.5 Majukumu ya Chama cha Ushirika

Kwa kuzingatia uwekezaji uliowekwa na Serikali katika mashamba ya BBT na kuhakikisha uendelevu wa mashamba hayo, ushirika utakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kusimamia uendeshaji wa shamba kwa mujibu wa mkataba ulioingiwa kati ya Wizara ya Kilimo na Ushirika wa BBT katika shamba husika;

ii. Kusimamia shughuli zote za uzalishaji katika mashamba ya pamoja;

iii. Kusimamia mapato na matumizi ya chama cha ushirika wa BBT ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za mapato na matumizi kwa wanachama kwa mujibu wa sheria ya Ushirika; na

iv. Kusimamia maendeleo ya ushirika kwa kwa mujibu wa sheria ya ushirika.

3.4.6 Majukumu ya Wanufaika wa Program ya BBT (Vijana)

Vijana wenye sifa waliodahiliwa katika Programu ya BBT wanawajibu wa kutekeleza yafuatayo:

i. Kushiriki mafunzo ya kilimo biashara yatakayoandaliwa na Wizara ya Kilimo;

ii. Kushiriki kikamilifu katika uzalishaji kwa kufuata kanuni bora za kilimo;

iii. Kushiriki shughuli za maandalizi ya mashamba ikiwemo kusafisha na kuweka miundombinu;

iv. Kutumia shamba alilopewa katika shughuli za uzalishaji wa mazao yaliyokusudiwa kama itakavyoelekezwa na

Wizara ya Kilimo kwa mujibu wa taarifa ya afya ya udongo;

v. Kurejesha shamba endapo atashindwa kuendelea na uzalishaji;

vi. Kutunza na kulinda miundombinu na mali zilizopo katika maeneo ya mafunzo na uzalishaji (mashamba ya BBT);

vii. Kushiriki mafunzo ya ukakamavu na uzalendo kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) yatakayoandaliwa;

viii. Kuzingatia taratibu na maelekezo yote yanayotolewa na Wizara ya Kilimo katika utekelezaji wa Programu ya BBT;

ix. Kulipa kodi, ushuru na tozo mbalimbali za Serikali ikiwemo kodi ya ardhi (land rent), ushuru wa mazao na kodi nyingine za Serikali kwa mujibu wa sheria;

x. Kujigharamia mahitaji muhimu ya kujikimu ikiwemo chakula, huduma afya, umeme na maji;

xi. Kushiriki katika shughuli za kijamii katika maeneo ya mradi;

xii. Kutopangisha shamba kwa mtu binafsi, taasisi au Kampuni katika kipindi chote cha mkataba wa upangishaji pamoja na masharti mengine yaliyoainishwa kwenye mkataba wa upangishaji;

xiii. Kutunza na kuhifadhi mazingira katika eneo la utekelezaji wa Programu ikiwemo udhibiti wa taka (viuatilifu na vifungashio vyake, vifungashio vya mbolea, mabaki ya mazao, vyakula), matumizi bora ya maji, nishati nk; na

xiv. Kutekeleza na Kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Serikali.

3.5 SABABU ZINAZOWEZA KUMWONDOA KIJANA KWENYE PROGRAMU YA BBT

Washiriki wanapaswa kuheshimu Sheria, taratibu na miongozo mbalimbali iliyowekwa katika kipindi chote cha mafunzo pamoja na utekelezaji wa Programu ya BBT. Zifuatazo ni sababu zinazoweza kumwondoa mshiriki katika Programu ya BBT: -

i. Kukosa nidhamu na utii kwa viongozi wa Serikali na kuheshimu wenzake;

ii. Kukiuka masharti ya mkataba wa upangishaji wa ardhi kati ya mnufaika na Wizara ya Kilimo;

iii. Kutokuwepo katika Kituo atamizi bila ruhusa;

iv. Ulevi;

v. Kuwa na tabia za wizi na tabia nyingine zisizokubalika katika jamii;

vi. Kutotekeleza wajibu wake kama mshiriki wa BBT ikiwemo kutokushiriki kazi za shamba bila kufuata utaratibu;

vii. Kuchochea vurugu, migomo na hali yoyote inayoweza kuhatarisha amani nautulivu katika eneo la mradi;

viii. Kuharibu miundombinu na vifaa kwa makusudi;

ix. Kutoa taarifa zisizo sahihi zinazo potosha na kuhujumu Programu ya BBT;

x. Kutokufuata Sheria, Kanuni na taratibu za Serikali katika vituo atamizi na katika eneo la mradi;

xi. Kutoa taarifa zinazohusiana na Programu ya BBT bila kufuata utaratibu; na

xii. Kuomba kusitisha ushiriki kwenye Programu.

4.0 HITIMISHO

Mwongozo huu umetolewa kwa kuzingatia Sheria za mamlaka mbalimbali zinazoongoza utekelezaji wa shughuli za uzalishaji, uuzaji na ununuzi wa mazao ya kilimo. Mwongozo umezingatia kuwa fedha zinazowekezwa ni fedha za umma hivyo unahitajika usimamizi thabiti. Mwongozo huu ni nyenzo muhimu ambayo itatumiwa na wadau katika utekelezaji wa Programu ya BBT. Aidha, Mwongozo huu ni wa miaka nane na unaweza kuboreshwa kwa kuzingatia mahitaji ya wakati husika ili kuimarisha utekelezaji wa Programu ya BBT na kuendeleza uzalishaji katika myororo wa thamani.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO NA. 1

Vigezo na Masharti kwa Washiriki katika Vituo Atamizi Vya Kilimo Biashara

i. Awe na umri kati ya miaka 18 - 40;

ii. Awe na mdhamini mwenye kitambulisho cha taifa au namba ya NIDA;

iii. Awe tayari kuishi katika kituo Atamizi wakati wote wa utekelezaji wa mafunzo;

iv. Awe tayari kushiriki mafunzo ya Kilimo Biashara bila kukatisha pasipo kuwa na sababu maalum;

v. Awe tayari kutii sheria za nchi;

vi. Awe tayari kutii kanuni, miongozo na taratibu za uendeshaji wa kituo husika;

vii. Awe na afya njema itakayomuwezesha kushiriki kikamilifu katika mafunzo (atawasilisha fomu ya vipimo kutoka katika hospitali inayotambuliwa na Serikali);

viii. Awe tayari kujitolea na kujifunza ujasiriamali;

ix. Haruhusiwi kuambatana na mtoto kwenye mafunzo;

x. Awe tayari kusimamia, kutunza na kulinda mali za Kituo; na

xi. Awe na Barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Serikali ya Kijiji/Mtaa.

KIAMBATISHO NA. 2

Kanuni na Taratibu za Kufuata Kijana Awapo Kituoni

i. Hairusiwi kuvuta sigara na unywaji wa pombe eneo la Kituo;
ii. Ni marufuku kuvuta bangi na matumizi ya madawa ya kulevya katika eneo la ndani na nje ya Kituo;
iii. Hairuhusiwi kutoka nje ya Kituo bila ruhusa ya uongozi wa kituo;
iv. Ni marufuku kupigana ndani na nje ya Kituo;
v. Ni marufuku kutumia au kutoa lugha za matusi ndani na nje ya Kituo;
vi. Hairuhusiwi kijana kuingia chumba cha jinsia tofauti;
vii. Hairuhusiwi kuacha kushiriki kazi atakazopangiwa na Kituo;
viii. Nimarufuku kuiba kitu chochote ndani na nje ya kituo;
ix. Hairuhusiwi kuacha kuingia darasani ama kushiriki vipindi bila ruhusa kutoka kwenye uongozi wa Kituo
x. Hairuhusiwi kutoa kauli za vitisho;
xi. Hairuhusiwi kumiliki silaha ya aina yoyote ile;
xii. Hairuhusiwi kulala chumba kimoja jinsia tofauti;
xiii. Hairuhusiwi kupika ndani ya chumba;
xiv. Hairuhusiwi kumiliki chombo cha umeme (Jagi la umeme, Heater); na
xv. Hairuhusiwi kushawishi, kuchocheo au kushiriki migomo.

KIAMBATISHO NA. 3

Mahitaji Muhimu ya Kijana Katika Vituo Atamizi na katika eneo la mradi

Mshiriki anatakiwa kuripoti kituoni akiwa na mahitaji yafuatayo:

i. Mashuka mawili;
ii. Blanketi moja;
iii. Fomu ya vipimo vya Daktari;
iv. Kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA;
v. Kadi ya Bima ya Afya inayofanya kazi kwa kipindi atakachokuwa kituoni na shambani
vi. Picha ndogo za rangi ya bluu (passport size) nne;
vii. Sabuni za kuogea;
viii. Sabuni za kufulia;
ix. Nguo za michezo;
x. Dawa ya meno na mswaki;
xi. Kandambili;
xii. Raba za michezo;
xiii. Ndoo ya kuogea;
xiv. Vyombo vya kulia chakula (sahani, bakuli, kikombe na kijiko);
xv. Kaunta book QR3, kalamu na rula;
xvi. Gumboot, overall (dark green), kofia za kukinga jua za duara;
xvii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa;
xviii. Barua ya utambulisho kutoka Serikali ya Kijiji au Mtaa;
xix. Chandarua 3 × 6; na
xx. Taulo.

bbt

Building a Better Tomorrow

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

AJENDA 10/30

KILIMO NI BIASHARA